# BARAZA LA WAWAKILISHI – ZANZIBAR

## ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

## **BARAZA LA KUMI LA WAWAKILISHI**

## **MKUTANO WA NNE**

**Kikao cha Tatu – Tarehe 10 Septemba, 2021.**
Kikao Kitaanza Saa 3.00 (Tatu) Asubuhi
na Dua zitasomwa.

**MASWALI:**

**Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, Sera, Uratibu na Baraza la Wawakilishi:**

121. MHESHIMIWA PROF. OMAR FAKIH HAMAD (Jimbo la Pandani) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, Sera, Uratibu na Baraza la Wawakilishi:

Kama ilivyo desturi kwa mabunge mengi duniani, kwa muda sasa, Serikali imeona busara kuendesha shughuli za Baraza la Wawakilishi katika Makao Makuu ya Zanzibar, Unguja Mjini, kuliko kuwa na baadhi ya mikutano katika kisiwa cha Pemba. Hata hivyo, kwa upande mwengine, imekuwa ni mzigo na gharama zaidi kwa Wawakilishi kutoka Pemba wawe wa kuchaguliwa, wa kuteuliwa au wa viti maalum.

(a) Je, Serikali inawatafautishaje kimaslahi na kistahiki Wawakilishi kutoka Pemba na wale kutoka Unguja kama inavyoelekezwa na Sheria za Utumishi.

(b) Je, Serikali haioni haja ya kuendelea kuughuisha na kuutunza ukumbi wa Baraza la Wawakilishi ulioko Pemba ili kuweza kukidhi haja pindi kukiwa na dharura ya kuendesha mikutano ya Baraza la Wawakilishi kisiwani Pemba.

**Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora:**

67. MHESHIMIWA YAHYA RASHID ABDULLA (Jimbo la Kwahani): Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora:

Kwa sasa sekta za kilimo, elimu na afya zimerejeshwa katika Wizara husika kutoka kwenye Ugatuzi.

(a) Je, stahiki za wafanyakazi kwa mfano nauli, malimbikizo ya likizo zitalipwa na nani.

(b) Je, wale maafisa waliokuwepo kwenye ugatuzi mfano, naibu wakurugenzi watarejeshwa kwenye sekta zao.

**Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ:**

112. MHESHIMIWA PROF. OMAR FAKIH HAMAD (Jimbo la Pandani) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ:

Pamoja na jitihada za Serikali kuhimiza huduma bora katika mamlaka husika za utoaji vyeti vya kuzaliwa na vitambulisho vya mzanzibari mkaazi, lakini bado suala la upatikanaji wa vyeti na vitambulisho limekuwa likilalamikiwa na watu kwa asilimia kubwa.

(a) Je, Serikali inafahamu kwamba watu wengi wanaosumbuliwa katika kupata vyeti na vitambulisho ni kwa kushindwa kulipia pesa zisizo halali katika huduma hii.

(b) Je, wafanyakazi wa Mamlaka hizi ni wafanyakazi wa Serikali au watumishi wa umma au wa kampuni zinazojitegemea au watu binafsi.

(c) Ni wapi na kwa utaratibu upi wananchi wanatakiwa kuripoti uonevu wanaofanyiwa katika kutafuta huduma za vyeti vya kuzaliwa na vitambulisho vya mzanzibari mkaazi.

**Ofisi ya Rais, Kazi, Uchumi na Uwekezaji:**

106. MHESHIMIWA SAADA RAMADHAN MWENDWA (Nafasi za Wanawake) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Kazi, Uchumi na Uwekezaji:

Katika kupunguza umaskini na kuongeza kipato kwa wanawake na watu wenye mahitaji maalum, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imekuwa na utaratibu wa kuwapatia mikopo kwa ajili ya kupunguza ukali wa maisha kwa makundi hayo. Kwa kuwa mikopo hiyo imekuwa inasaidia sana na kwa vile wanaohitaji mikopo hiyo ni wengi.

(a) Je, ni kiasi gani cha fedha kimetolewa kwa mahitaji ya mikopo kwa mwaka 2020/2021.

(b) Ni vikundi vingapi vya kina mama vya Mkoa wa Mjini Magharibi wamepata mikopo hiyo kwa mwaka 2020/2021.

**Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo:**

101. MHESHIMIWA HUDHAIMA MBARAK TAHIR (Nafasi za Wanawake) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo:

Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar katika kipindi cha miaka mitano (5) iliyopita ilifanya jitihada kubwa sana ya kupongezwa katika kukuza sekta ya habari nchini na kuwasaidia wananchi wake kuweza kupata habari kwa urahisi.

(a) Shirika la ZBC kupitia mradi wa Z-Mux, wamenufaikaje kupitia pato la moja kwa moja linalotokana na gharama kubwa iliyotumika katika uwekezaji huo.

(b) Je, Wizara ina mpango gani wa kuwapunguzia wananchi gharama za malipo yanayotokana na matumizi ya ving’amuzi vya Z-Mux ili wananchi waweze kupata habari kwa urahisi.

(c) Je, kuna changamoto gani zinazopatikana katika kukabiliana na ushindani uliopo katika upatikanaji wa habari.

**Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji:**

54. MHESHIMIWA MOH'D MGAZA JECHA (Jimbo la Mtambile) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi:

Kwa kipindi kirefu hivi sasa, wananchi wa Zanzibar hususan madereva vijana huwa na desturi ya kupita barabarani wakiendesha vyombo vya moto vinavyopiga zogo na hatimae kuchafua hali ya hewa (noise pollution) pasi na kuwa na sababu ya msingi.

(a) Je, ni madereva wangapi wameshakamatwa kwa kufanya kosa hilo hadi sasa kwa kipindi cha Januari hadi Agosti, 2021.

(b) Kwanini kila siku vitendo hivyo viovu vinazidi kuongezeka na baadhi ya wakati hufanyika mbele ya askari Polisi.

(c) Je, ni hatua gani zinazochukuliwa kwa mafundi ambao huyatoboa kwa makusudi mabomba ya kutolea moshi ili kuwakera wananchi wetu, madereva wengine na wale wanaokaa karibu na barabara.

85. MHESHIMIWA BAKAR HAMAD BAKAR (Jimbo la Wawi) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi:

Kwa kuwa Serikali imewazuia wananchi wa vijiji vya Furaha, Mvumoni na maeneo mengine yaliyozunguka Uwanja wa Ndege - Pemba kwa ajili ya upanuzi wa Uwanja huo, na kwa kuwa siku nyingi zimepita na hakuna hatua yoyote iliyochukuliwa na Serikali katika kuliendeleza eneo hilo.

Je, kwa nini Serikali isiwaruhusu wananchi wa maeneo hayo kuendelea na shughuli zao ikiwa ni pamoja na uendelezaji wa nyumba zao za kuishi mpaka pale itakapokuwa tayari kwa ujenzi wa Uwanja huo.

**Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi:**

70. MHESHIMIWA YAHYA RASHID ABDULLA (Jimbo la Kwahani)- Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Uchumi wa Buluu na Uvuvi:

Katika uchumi wa buluu shughuli nyingi sana zitafanywa katika maeneo ya bahari ikiwemo uchimbaji wa mafuta, madini, ufugaji wa samaki na uvuvi. Kila moja katika shughuli hizo itadai nafasi yake.

(a) Je, Zanzibar imeshaandaa mipango ya mazingira ya habari "M.S.P" (Marine Special Planning).

(b) Je, Zanzibar imejipangaje katika usimamizi wa mazingira ya bahari.

(c) Je, utafiti juu ya mipango ya mazingira ya baharini (Marine Special Planning) umefanyika Zanzibar.

91. MHESHIMIWA SHAIB HASSAN KADUARA (Jimbo la Chake Chake) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Uchumi wa Buluu na Uvuvi:

Katika kuhakikisha uzalishaji wa samaki unaongezeka na kuwaondolea wananchi wetu shida ya kitoweo na matumizi mengine ya samaki hapa Zanzibar, Serikali imekuja na mpango wa ufugaji wa samaki unaohakikisha kuna ongezeko la kutosha la vifaranga vya samaki, ambavyo ndio msingi wa uzalishaji wa samaki hao.

(a) Je, Serikali imefikia wapi kwenye mpango wa uzalishaji wa vifaranga vya samaki hapa Zanzibar.

(b) Je, Serikali inakusudia kuwaaminisha wananchi wake kuwa, uzalishaji wa samaki hauna tija tena kwa matumizi ya samaki hao hapa nchini.

**Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali:**

10. MHESHIMIWA SHAMATA SHAAME KHAMIS (Jimbo la Micheweni) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali:

Sekta ya elimu ni chanzo cha mafanikio kwa nyanja zote za kimaisha. Hata hivyo, sekta hii bado imekuwa na changamoto nyingi hasa kwa mikakati inayofanywa na skuli husika.

(a) Je, katika kuendeleza lengo hilo la ufaulu, Wizara ina mkakati gani wa kuendesha mitihani ya MOKO ili kusaidia kufanikisha azma hiyo njema.

(b) Je, mpaka sasa skuli ngapi kwa Zanzibar zimeshaanza na utaratibu huu.

(c) Kwa skuli zilizoanzisha utaratibu huu, ni kitengo gani au ni nani anapaswa kugharamia mitihani ya aina hiyo.

35. MHESHIMIWA AZZA JANUAR JOSEPH (Nafasi za Wanawake) Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali:

Naipongeza Serikali kwa hatua iliyofikia ya kutoa mikopo kwa wanafunzi wa elimu ya juu. Serikali imefanikiwa kuwasomesha wanafunzi wengi ambao hadi sasa hawajapata ajira, hali inayokwamisha zoezi zima la urejeshaji wa mikopo hiyo.

(a) Je, Serikali ina mpango gani wa kuwapatia ajira wahitimu hao ili waweze kurejesha fedha waliyokopeshwa.

(b) Je, Serikali inatumia mbinu gani za kuwatambua wahitimu hao wote mara tu wanapopata ajira ili waweze kurejesha fedha hizo.

**<u>Wizara ya Maji, Nishati na Madini:</u>**

13. MHESHIMIWA MACHANO OTHMAN SAID (Jimbo la Mfenesini) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji, Nishati na Madini:

Wakati wa ziara ya Mheshimiwa Waziri wa Maji, Nishati na Madini katika Jimbo la Mfenesini, Mamlaka ya Maji Zanzibar (ZAWA) iliwaahidi wananchi wa Mwachaalale, Mwakaje na Kilindi, kwamba watavimalizia visima vitatu vya Mwachealale, Selem na Meli nane ambavyo vilichimbwa kupitia mradi wa Ras-el-khema. Hata hivyo, ni zaidi ya miezi minne sasa imepita hakuna hatua zozote zilizochukuliwa za kutekelezwa ahadi hiyo.

(a) Kwa kuwa wananchi wa maeneo hayo wanapata shida kubwa ya maji safi na salama, ni lini Serikali itatekeleza ahadi yake hiyo.

(b) Ni gharama ya kiasi gani inatarajiwa kutumika katika kukamilisha visima hivyo.

**Wizara ya Afya, Ustawi wa Jamii, Wazee, Jinsia na Watoto:**

78. MHESHIMIWA HABIB ALI MUHAMED (Jimbo la Mtambwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Afya, Ustawi wa Jamii, Wazee, Jinsia na Watoto:

Zipo baadhi ya taasisi na mashirika ya umma yamewakatia bima (NHIF) ya afya wafanyakazi wao ili waweze kupata huduma iliyokuwa bora.

Je, ni sababu gani zinazopelekea wagonjwa kutopata dawa zote walizoandikiwa na daktari katika chumba cha kutolea dawa ikiwemo hospitali ya Mnazi Mmoja ambao wamekatiwa bima na waajiri wao.

145. MHESHIMIWA MWANAASHA KHAMIS JUMA (Jimbo la Dimani) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Afya, Ustawi wa Jamii, Wazee, Jinsia na Watoto:

Kumekuwa na malalamiko kwa baadhi ya wanafunzi wanaosoma chuo cha Afya cha Muhimbili (MUHAS) wanaotoka Wizara ya Afya Zanzibar kucheleweshewa posho za kujikimu kwa mwaka wa masomo 2020/2021 huku hali yao ya maisha ikiwa ngumu na gharama za mahitaji yao kuwa kubwa.

(a) Je, Wizara imechukua hatua gani kusawazisha hali hiyo.

(a) Kwa vile wanafunzi hawa wameshaandika barua Wizarani muda mrefu bila ya kupewa mrejesho, Je, Wizara ina mpango gani wa kuwapatia posho zao kwa haraka.

**Wizara ya Biashara na Maendeleo ya Viwanda:**

88. MHESHIMIWA SHAIB HASSAN KADUARA (Jimbo la Chake Chake) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Biashara na Maendeleo ya Viwanda:

Tunaishukuru sana Serikali kwa kuliruhusu Shirika letu la Biashara la Taifa la Zanzibar (ZSTC) kuanzisha jengo lake kisiwani Pemba, katika Jimbo la Chake Chake. Kukamilika kwa jengo hilo, kungelisaidia sana kuimarisha huduma za Shirika hili na kuwasaidia wananchi wetu kupata huduma hizo kwa urahisi. Hata hivyo, jengo hilo lililokusudiwa kujengwa limekwama katika hatua za awali kwa muda mrefu sasa.

(a) Je, kuna sababu zipi za msingi zilizopelekea jengo hilo kukwama tokea lilipoanza kujengwa.

(b) Je, Serikali ina mpango gani wa kulikamilisha jengo hilo ili liweze kutoa huduma zilizokusudiwa.

**Wizara ya Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo:**

43. MHESHIMIWA KOMBO MWINYI SHEHE (Jimbo la Wingwi) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo:

Kwa kuwa nchi yetu ya Zanzibar inaagiza bidhaa nyingi za nafaka na matunda zikiwemo mbatata na vitunguu kutoka Tanzania Bara. Na kwa kuwa bidhaa hizo huletwa kwa kutumia magunia na mapolo ambayo hushonewa kwa kutumia majani tofauti tofauti kutokea huko.

Je, Serikali haioni kuwa majani hayo yanaweza kupelekea maradhi mbali mbali kwa mimea yetu hapa Zanzibar.

**Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makaazi:**

96. MHESHIMIWA KOMBO MWINYI SHEHE (Jimbo la Wingwi) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ardhi na Maendeleo ya Makaazi:

Katika eneo la Mtemani Wete mkabala na ukumbi wa Baraza la Wawakilishi mwelekeo wa barabara ya Konde, kuna jengo ambalo upande mmoja unamilikiwa na mtu binafsi na upande wa pili unamilikiwa na Serikali. Kwa kuwa jengo hilo lilijengwa wakati mmoja likiwa na wamiliki wawili tofauti na kwa kuwa nyumba inayomilikiwa na mtu binafsi iko imara, na nyumba ya Serikali ni mbovu na imekuwa kama gofu ambalo linahatarisha maisha ya wakaazi wa eneo hilo.

(a) Je, Mheshimiwa Waziri unaweza kulieleza Baraza hili tukufu kwamba, ni sababu zipi zilizopelekea nyumba hii ya Serikali kuwa katika hali hiyo.

(b) Je, ni kwanini Serikali inashindwa na mtu binafsi katika kuitunza nyumba hii.

(c) Je, ni lini Wizara imepanga kuifanyia marekebisho nyumba hii pamoja na nyumba nyengine za Serikali zenye sura kama hii ili kunusuru maisha ya raia wetu.

137. MHESHIMIWA PROF. OMAR FAKIH HAMAD (Jimbo la Pandani) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ardhi na Maendeleo ya Makaazi:

Serikali inastahili pongezi katika juhudi zake za kutatua migogoro ya ardhi nchini. Hata hivyo, kuna baadhi ya Masheha wanarejesha nyuma juhudi za Serikali, kwa kuzuia utaratibu wa kupatikana hati za viwanja kikiwemo cha Bwana Hamad Ali Hamad (maarufu Mkeka) katika kijiji cha Kibendera ndani ya jimbo la Pandani.

(a) Je, ni ipi juhudi ya Serikali katika kijiji cha Kibendera kuhakikisha kwamba wamiliki wenye umiliki wa asili wanapatiwa hati zao zilizokwamishwa na Sheha.

(b) Je, ni kwa nini Serikali kupitia Sheha inampa haki zaidi mtoto kwenye madai ya kiwanja alichouza baba yake wakati yeye mtoto akiwa mdogo.

**Zanzibar,**
**10 Septemba, 2021.**

**(Raya Issa Msellem)**
**KATIBU WA BARAZA.**